# MATANGAZO YA DOMINICA YA 5 YA PASAKA MWAKA 'B'– 28/04/2024

**1.** Waamini mnakumbushwa kushusha vibao vya kupigia magoni taratibu ili kuimarisha utulivu wa ibada.

**2.** Kamati Tendaji ya Uwaka K/Ndege inawatangazia wanaume wote Parokiani kushiriki Misa ya Mt. Yoseph Mfanyakazi itakayo fuatiwa na semina itakayo fanyika tarehe 4/5/2024 siku ya jumamosi saa kumi jioni katika ukumbi wa Inyasi.

**3.** Waamini mnakumbushwa kurudisha bahasha za Zaka za mwezi wa Nne, kwani muda umeisha.

**4.** Tarehe 1/5/2024 kutakuwa na Misa ya Mei Mosi, Misa itaanza saa 1:00 asubuhi. Katika Misa hiyo wafanyakazi pamoja na wanafunzi mnaombwa kuja na vifaa vyenu vya kufanyia kazi ili vibarikiwe. Pia kwa wale watakao kuwa na vipaji na shukrani mbalimbali mnaombwa kuja navyo. Hakutakuwa na Misa ya saa 12:30 asubuhi.

**5.** Tarehe 1/5/2024 tutakuwa na misa ya uzinduzi wa mwezi wa mama Bikira Maria saa 11:00 jioni. Kabla ya Misa tutakuwa na sala ya Rosali kuanzia saa 10:00 Jioni.

**6.** Jumanne tarehe 30/4/2024 kutakuwa na Semina katika Kroto kuhusu Mama Bikira Maria kuanzia saa 10:00 jioni.

**7.** Jumuiya za zamu mnaombwa kuleta vibaji vya chakula zaidi kama Unga wa ugali, unga wa ngano, sukari, mchele, maharage na vingine ili tusaidie wahitaji wa parokia.

**8.** Leo mara baada ya Misa ya pili, Masista watawapelekea wagonjwa na wazee Ekaristi Takatifu kwenye Jumuiya zifuatazo **MT. GABRIEL MALAIKA MKUU, MT. ANDREA BOBOLA, WAT. JOACKIMU NA ANNA, MT. URSULA, MT. THERESIA WA MTOTO YESU, MT. PHILIP EVANS.Jumapili Ijayo wajiandae Jumuiya zifuatazo**: MT. STANSLAUS KOSTIKA, MT. FRANCIS JEROME, MT. AGATHA, KRISTU MFALME, MT. JEAN MARIA MUZEEY, MOYO MTAKATIFU WA YESU. Mama na baba huruma mnaombwa kuwachukua Masista karibu na Sakristia.

**9.** Tunashukuru Jumuiya ya **MT. GABRIEL MALAIKA MKUU** na **MT. JEAN MARIA MUZEEY** kwa kazi nzuri ya usafi na kusimamia utaratibu wa Ibada. Juma lijalo ni zamu ya Jumuiya ya **(A) MT. YOHANE WA MSALABA** na **(B) MT. PAULO MTUME.** Jumuiya ya **MT. ALPHONCE RODRIGUEZ** na **MT. AUGUSTINO** wajiandae.

**10. NDOA. (SOMA MATANGAZO YA "KWA MARA YA KWANZA TU")**

a) Kwa mara ya **Kwanza**: Ndg. **Basil Ndetembea**, baba yake ni **Joseph Kirango** na mama yake ni **Antonia Simon** anataka kufunga ndoa na **Suzana Ernest**, baba yake ni **Ernest Muhemeli** na mama yake ni **Mkatale Sigani.** Wote wanasali katika parokia ya **Kristu Mfalme - Tabata**, **Jimbo Kuu la Dar-es-Salaam.**

b) Kwa mara ya **Kwanza**: Ndg. **Deogratias Mutekanga**, baba yake ni **Charles Sililo** na mama yake ni **Leticia John** anataka kufunga ndoa na **Rozaria Sikuku**, baba yake ni **Stanslaus Dakho** na mama yake ni **Anastazia Daati.** Wote wanasali katika Parokia ya **Paulo wa Msalaba**, **Jimbo Kuu la Dodoma.**

c) Kwa mara ya **Kwanza**: Ndg. **Sebastian Mathias**, baba yake ni **Mathias Lubinsha** na mama yake ni **Eva Lameck** anataka kufunga ndoa na **Jackline Adelbert**, baba yake ni **Adelbert Kakoko** na mama yake ni **Sophia Charles.** Wote wanasali katika parokia ya **St. Joseph Cathedral``**, **Jimbo Kuu la Dar-es-Salaam**

d) Kwa mara ya **Pili**: Ndg. **Christopher Lejeto**, baba yake ni **Richard Mazengo** na mama yake ni **Secilia Chidawali** anataka kufunga ndoa na **Juliana Mumbii**, baba yake ni **Mande Mumbii** na mama yake ni **Elizabeth Mumbii.** Wote wanasali katika parokia ya **Mt. Inyasi wa Loyola Kigango cha Peter Clavery**, **Jimbo Kuu la Dodoma.**